
TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Norway yaahidi NOK Milioni 30 ili kuimarisha Usalama wa chakula nchini Tanzania

Septemba 6, 2023, Dar es Salaam – Norway, kwa ushirikiano na Umoja wa Mataifa, inaongeza msaada wake kuimarisha Usalama wa Chakula nchini Tanzania. Ubalozi wa Norway na Umoja wa Mataifa nchini Tanzania wanafuraha kutangaza mchango wa ziada wa NOK Milioni 30 (takriban TZS Bilioni 7) kutoka Norway kwenda kwenye mfuko wa fedha wa kuchochea utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo endelevu (Tanzania SDG Acceleration Fund). Ahadi hii inategemewa kuimarisha miradi ya Umoja wa Mataifa inayolenga kuimarisha Usalama wa Chakula nchini Tanzania.

Mchango huu unakuja wakati muhimu ambapo dunia inakabiliana na athari za mivutano ya kijipolitiki, ikiwa ni pamoja na vita nchini Ukraine. Kwa kutambua uzito wa hali ambayo watu ulimwenguni wanakabiliana nayo, Norway imejitolea kwa haraka jumla ya NOK Bilioni 5 (takriban TZS Trilioni 1.2) kote ulimwenguni, ikisisitiza dhamira yake ya kusaidia wale wanaoathiriwa.

"Usalama wa chakula ni kipaumbele cha juu kwa Norway. Tunataka kusaidia Tanzania na Afrika nzima katika uzalishaji wa chakula. Kusaidia wakulima wadogo, wanawake, na kuwekeza katika mlolongo wa thamani wa uzalishaji wa chakula ni muhimu ili kufanikisha hili. Tunataka kuongeza usalama wa chakula nchini Tanzania kwa kuzingatia muktadha w anchi. Ninafurahi kuimarisha ushirikiano wetu na Umoja wa Mataifa nchini Tanzania kupitia mchango huu wa nyongeza," alisema Bi. Anne Beathe Tvinnereim, Waziri wa Maendeleo ya Kimataifa wa Norway ambaye kwa sasa yuko Tanzania akishiriki katika Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika.

"Tunashukuru sana Serikali na wananchi wa Norway kwa nyongeza hii ambayo itachangia katika kuimarisha nguzo muhimu ya kazi zetu na kuhakikisha kwamba Tanzania inaendelea kuwa na uhakika wa chakula," alisema Bw. Zlatan Milisic, Mratibu Mkaazi wa Umoja wa Mataifa nchini Tanzania. "Michango kama hii inaongeza juhudhi za pamoja katika kuhakikisha kwamba hakuna mtu anayeachwa nyuma, haswa katika nyakati hizi za changamoto."

Mchango wa Norway utaimarisha uwezo wa Umoja wa Mataifa kuhakikisha Watanzania wanapata chakula salama na bora kama ilivyoainishwa na lengo la pili la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG 2), ambayo yanakusudia kumaliza njaa, kufikia usalama wa chakula na lishe bora, na kukuza kilimo endelevu ifikapo mwaka 2030.

Note to Editors

Mfuko wa fedha wa kuchochea utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo endelevu (Tanzania SDG Acceleration Fund) ni jitihada ya pamoja kati ya Umoja wa Mataifa na Serikali ya Tanzania ambayo inalenga kukusanya na kuelekeza rasilimali zilizokusanywa kwenye miradi yenyе matokeo kubwa ili kuharakisha utekelezaji wa maendeleo ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) nchini Tanzania, na jitihada maalum za kuhakikisha kwamba hakuna mtu anayeachwa nyuma.

Kwa habari zaidi, tafadhali wasiliana na:

Karen-Emilie Asla

Adviser, Private Sector, Media & Communication

Royal Norwegian Embassy

Mobile: +255 754 328 645

Office: Norwegian Embassy, Dar es Salaam

Website: www.norway.no/en/tanzania

Facebook: [Norway in TZ](#)

X: [@NorAmbTZ](#)

Instagram: [@norwayintz](#)

Mr. Edgar Kiliba

Communication Analyst

United Nations Resident Coordinator's Office in Tanzania

Mobile: +255 692 890 077

Website: tanzania.un.org

Facebook: [United Nations Tanzania](#)

X: [@UnitedNationsTZ](#)

Instagram: [@unitednations_tz](#)